# *Waraka wa Sala wa Mwezi Machi 2026*

## NIA ZA SALA ZA BABA MTAKATIFU

Kila mwezi, Baba Mtakatifu huukabidhi Mtandao wake wa Sala Ulimwenguni nia za sala. Nia hizi hutuelekeza kujiunga naye katika kujali utu na utume wa kanisa. Nia hizi ni wito kwa ulimwengu wote kuziweka sala zetu katika matendo mahsusi; ni dira ya utume wa huruma kwa ulimwengu.

*Nia ya Sala ya Papa, Machi 2026:*

**Kwa upokonyaji silaha na amani:** Tusali ili mataifa yaelekee upande wa kukomesha matumizi ya silaha, hasa silaha za nyuklia, na kwamba viongozi wa dunia wachague njia ya mazungumzo na diplomasia badala ya matumizi ya nguvu.

## SALA YA MWEZI MACHI 2026

*Kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.*

Bwana wa Uzima,
ambao umemfanya kila mwanadamu kwa sura na mfano wako,
tunaamini kwamba umetuumba kwa ajili ya ushirika, sio kwa vita,
kwa udugu wa kibinadamu, si kwa uharibifu.

Wewe uliyewasalimia wanafunzi wako kwa maneno haya, Amani iwe nanyi.
Utupe amani yako, na nguvu ya kuifanya kuwa ukweli katika historia.
Leo tunainua sala yetu kwa ajili ya amani duniani,
kuyataka mataifa kuachana na silaha zao
na kuchagua njia ya majadiliano na diplomasia.

Zuia mioyo yetu ya chuki, uhasama, na kutojali,
ili tuweze kuwa vyombo vya upatanisho.
Tusaidie kuelewa usalama wa kweli
hauzaliwi kutokana na udhibiti unaochochewa na woga,
bali kutokana na uaminifu, haki, na mshikamano kati ya watu.
Bwana, waangazie viongozi wa mataifa,
ili wawe na ujasiri wa kuacha mipango ya kifo,
kusimamisha mashindano za silaha,
na kutoa kipaumbele kwa maisha ya walio wanyonge zaidi.
Tishio la nyuklia lisiamue tena mustakabali wa wanadamu.

Roho Mtakatifu,
utufanye kuwa wajenzi waaminifu na wabunifu wa amani ya kila siku:
katika mioyo yetu, katika familia zetu,
katika jamii zetu na katika miji yetu.
Kila neno la fadhili, kila ishara ya upatanisho,
na kila chaguo la majadiliano liwe mbegu ya ulimwengu mpya. **Amina.**

## SALA YA MAJITOLEO YA KILA SIKU

Ee Baba mwema, natambua uko hapa pamoja nami.
Nakuja mbele yako katika siku hii mpya.
Weka moyo wangu kwa mara nyingine tena
karibu na Moyo wa Mwanao Yesu,
anayejitoa kwa ajili yangu na anayekuja kwangu katika Ekaristi.
Roho wako Mtakatifu anifanye kuwa rafiki na mtume wake,
aliye tayari kwa utume wake wa huruma ulimwenguni.

Ninaweka mikononi mwako furaha na matumaini yangu,
kazi zangu na maumivu yangu, mimi mzima na kila kitu nilichonacho,
kwa kushirikiana na kaka na dada zangu
wa Mtandao huu wa Sala Ulimwenguni.

Pamoja na Mama Maria, ninakutolea siku yangu
kwa ajili ya utume wa Kanisa
na kwa nia ya Sala ya Baba Mtakatifu [na Askofu wangu] kwa mwezi huu. **Amina**.

### Mtazamo wa Moyoni:

Kataa silaha na ugomvi, utoe nafasi kwa majadiliano, uwe chombo cha amani.

Amani ya kweli huzaliwa na moyo wa mapatano. Kupanda mbegu ya amani ulimwenguni kunaanza na kuiishi amani katika maisha ya kila siku. Upokonyaji wa silaha unaoyabadili mataifa unaanza kwa upokonyaji wa silaha ndani yetu.

*Nukuu*: Hatua ya 3, **Nyia ya Moyo** – *Kuchagua njia za maisha*. Kukana njia zinazoelekea kwenye mauti).

---

Mtandao wa Sala wa Baba Mtakatifu Ulimwenguni ni Ushirika wa Kipapa (Pontifical Society), wenye kazi ya kuwahamasisha Wakatoliki kukabili changamoto za ulimwengu na za utume wa Kanisa, kwa njia ya sala na matendo mema. Changamoto hizi hutolewa kila mwezi kwa Kanisa lote, kupitia nia za sala za Baba Mtakatifu.

Mtandao wa sala wa Baba Mtakatifu Ulimwenguni ulianzishwa mwaka 1884 kama "Utume wa Sala". Chimbuko lake hasa ni hamu kubwa waliyokuwanayo watu ya kushiriki kazi ya kimisionari; lakini si wote wangeweza kusafiri mbali kwa ajili ya kazi za kimisionari. Jibu likawa kwamba wangeweza kushiriki katika kazi za kimisionari hapo walipo kwa sala; hasa wakiwaombea wamisionari na Kanisa, na kwa kuuishi vema Ukristo wao, tena kwa majitoleo yao ya kila siku. Kwa sasa utume huu upo katika nchi 92 na una zaidi ya Wakatoliki milioni 22. Utume huu unajumuisha tawi lake la vijana linaloitwa Vijana Wana-Ekaristia (EYM, Eucharistic Youth Movement).

**JUKUMU LETU:** Kutumia sala na matendo mema kama njia ya kukabiliana na changamoto za wanadamu na za utume wa Kanisa. **LENGO LETU:** Kuchangia katika kuutakatifuza ulimwengu kwa kuzisali na kuziishi nia za sala za Baba Mtakatifu. **UTUME WETU:** Kuwa mitume wa Kristo katika maisha ya kila siku kwa kupitia njia ya kiroho inayoitwa "Njia ya Moyo". Njia hii hubadilisha maisha yetu kuwa kwa ajili ya utume wa Kristo, utume wa huruma kwa ulimwengu.

POPE'S WORLDWIDE PRAYER NETWORK & EUCHARISTIC YOUTH MOVEMENT,
**St Francis Xavier Parish, Nyakahoja, P. O. Box 266 Mwanza, Tanzania**
+255 766 333833 +255 754 865401 popesprayer@aorjesuits.org salinapapa.or.tz